# Bring report on breaches of contract, NARCO told

By Guardian Reporter, Handeni

LIVESTOCK and Fisheries deputy minister, Pauline Gekul has given seven days to the National Ranching Company Limited (NARCO) to submit report on how it has implemented government directives which among others required the management to take actions against investors who have violated contract terms.

Gekul gave the order in Handeni District on Saturday during her tour to inspect operations of the Mzeri ranch which is under NARCO. She said the Livestock and Fisheries Minister Mashimba Ndaki had earlier directed the management to take actions against block owners by February 15, this year.

She said the minister had even wanted NARCO to re-possess all the undeveloped blocks within its ranches.

"The minister had already directed you to take actions against all those who have failed to develop the blocks; but nothing has been done so far. I want you to submit the report within seven days," said the Deputy Minister.

Gekul faulted the management over poor supervision of the blocks which has resulted in the government losing revenues. She said block owners must be ordered to present to NARCO their payment plans as well as stating on when they complete their payments.

She however challenged NARCO to improve production of best cattle breeds to be distributed to livestock keepers for production of quality meat, milk and other dairy products. She said livestock keeping in NARCO ranches should be conducted in modern ways to ensure production of quality raw materials to be supplied to available factories.

Livestock is a key agricultural sub-sector in the country. About 36-per cent of farm households are engaged in livestock-keeping, one per cent as fully livestock farmers and 35per cent as crop-livestock mix farmers.

*Despite Tanzania being among* African countries that have large numbers of livestock, it is yet to tap the potential.

Scanned with CamScanner

# Fishermen embrace value addition drive

By Polycarp Machira, Kigoma

FISHERIES stakeholders in Kigoma region have welcomed a new initiative to improve the sustainability of fishing in Lake Tanganyika, expecting that it will boost their economies.

The region is earmarked to benefit from the euro 3m/- project in value chain addition to fresh water sprat, perch and dry sardine fished in Lake Tanganyika, making Tanzania among 10 countries picked for a project named 'Fish 4ACP,' grouping countries in the Africa, Caribbean and Pacific zone, in partnership with the UN Food and Agriculture Organization (FAO).

> **It is my hope that implementing the project will solve the problems and challenges we face," he said, airing the view that the focus is to explore global markets as they demand quality products.**

The five-year project is managed by the Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI) and aims at giving fishermen skills to increase production and reduce post fish harvest losses before the catch reaches the market.

Speaking to reporters on a study visit, the stakeholders were of the view that if well managed, fishing activities in the lake can vastly contribute to the region's economic uplift.

Frank Kibiti, a regional official in charge of fish quality control and marketing, noted that there are great investment opportunities in value chain addition, which can increase revenues.

He said the Fish4ACP project

TURN TO PAGE 2

Scanned with CamScanner

# NARCO yapewa siku 7 kutoa maelezo mkataba vitalu

**Na Mbaraka Kambona,**
HANDENI

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ameipa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), wiki moja kueleza walivyotekeleza agizo alilotoa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki la kuwachukulia hatua waliokiuka mkataba wa umiliki wa vitalu katika ranchi hizo.

Gekul alitoa agizo hilo alipokagua shughuli za Ranchi ya Mzeri iliyopo katika Halmashauri ya Mji, Handeni juzi.

Alisema kuwa Waziri Ndaki alishatoa maelekezo kwa Kampuni hiyo kuwa mpaka Februari 15 wawe wameshachukua hatua kwa walioshindwa kuendeleza vitalu walivyopangishwa ikiwamo kuwanyang'anya.

"Ndugu zangu mheshimiwa waziri alishatoa maelekezo kuhusu waliokiuka mkataba, leo ni Februari 27 (juzi), hatujapata taarifa yoyote, natoa wiki moja tupate taarifa ya utekelezaji, kauli ilishatolewa tunataka utekelezaji, vinginevyo tutaona NARCO hamtoshi," alisema Gekul.

Alisema kuwa kwa muda mrefu kumekuwa hakuna ufuatiliaji wa kina kuhusu ranchi hizo na watu kugeuza kichaka na serikali imeendelea kupoteza mapato yake.

Gekul alisema walioonesha nia ya kuanza kulipa wanaweza kuvumiliwa, lakini waeleze wanampango gani na deni watamaliza lini, lakini ambao mpaka sasa hawajafanya lolote watafutwe na wachukuliwe hatua.

Pia, aliwataka NARCO kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na maziwa ili kukidhi mahitaji ya viwanda na kuuza nje ya nchi.

"Tunataka wawekezaji watakaofuga kibiashara katika ranchi zetu, huku hatutaki kufuga kama maonyesho, tunataka ufugaji kwenye hizi ranchi uwe wa tija ili mazao yaende yakachakatwe kwa wingi katika viwanda vyetu," alifafanua Gekul.

Alisema kuwa serikali imepunguza gharama za ukodishaji wa vitalu na sasa ni Sh. 3,500 kwa heka moja, aliwahamasisha wawekezaji ambao wana nia ya kufuga kisasa kutumia fursa hiyo kuendesha ufugaji wa kisasa katika ranchi hizo ili kuongeza tija katika uzalishaji na kuongeza pato la taifa.

Scanned with CamScanner

## KIKAO CHA KAZI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Ummy Mwalimu (mwenye kilemba), akizungumza na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (wapili kulia), baada ya kikao cha wavuvi na naibu waziri huyo, mjini Tanga, juzi. Wa tatu kulia ni Mkuu wa Wuilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa.



Scanned with CamScanner

# NARCO yapewa siku 7 kueleza ilivyotekeleza maagizo ya serikali

**Na MBARAKA KAMBONA,** *Handeni*

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ameipa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), wiki moja kueleza namna ilivyotekeleza maagizo aliyoyatoa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kuwachukulia hatua wale wote waliokiuka mkataba wa umiliki wa vitalu katika ranchi hizo.

Pauline, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita, alipotembelea kukagua shughuli za Ranchi ya Mzeri, iliyopo katika Halmashauri ya Mji, Handeni.

Alisema Waziri Ndaki alishatoa maelekezo kwa kampuni hiyo kuwa, mpaka itakapofika Februari 15, mwaka huu, wawe wameshachukua hatua kwa walioshindwa kuendeleza vitalu walivyopangishwa, ikiwemo kuwanyang'anya vitalu hivyo.

"Ndugu zangu, waziri alishatoa maelekezo kuhusu waliokiuka mkataba, leo ni Februari 27, hatujapata taarifa yoyote, natoa wiki moja tupate taarifa ya utekelezaji, kauli ilishatolewa, tunataka utekelezaji, vinginevyo tutaona NARCO hamtoshi," alisema.

Aliongeza: "Kwa muda mrefu kumekuwa hakuna ufuatiliaji wa kina kuhusu ranchi hizo na watu kugeuza kichaka na serikali imeendelea kupoteza mapato yake, jambo ambalo haturuhusu liendelee kutokea."

Alisema wale ambao wameshaonesha nia ya kuanza kulipa, wanaweza kuvumiliwa, lakini waeleze wana mpango gani na deni watamaliza lini, lakini ambao mpaka sasa hawajafanya lolote, watafutwe na wachukuliwe hatua.

Aidha, aliwataka NARCO kuhakikisha wanaongeza uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na maziwa ili kukidhi mahitaji ya viwanda na kuuza nje ya nchi.

"Tunataka wawekezaji watakaofuga kibiashara katika ranchi zetu, hatutaki kufuga kama maonesho, tunataka ufugaji kwenye hizi ranchi uwe wa tija ili mazao yaende yakachakatwe kwa wingi katika viwanda vyetu," alifafanua

Alisema serikali imepunguza gharama za ukodishaji wa vitalu na sasa ni sh. 3,500, kwa heka moja, hivyo aliwahamasisha wawekezaji, ambao wana nia ya kufuga kisasa, kutumia fursa hiyo kuendesha ufugaji wa kisasa katika ranchi hizo ili kuongeza tija katika uzalishaji na kuongeza pato la taifa.

**MNADANI**



...Halmashauri ya Mji Handeni, mkoani

# Machinjio Vingunguti kuingiza bil 4/-, kutoa ajira 3,000

Na Oscar Job

JIJI la Dar es Salaam linatarajiwa kuingiza zaidi ya Sh bilioni 4 kwa mwaka kutoka kwenye Machinjio ya kisasa ya Vingunguti, yanayotarajia kuanza kazi Machi mwaka huu.

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri amesema kuwa uongozi wa jiji hilo, umefanya mchakato wa kuagiza magari maalumu ya kubebea nyama kwa ajili ya kuzisambaza kwa walaji.

Shauri aliieleza HabariLEO jana kuwa machinjio hiyo itakapoanza kazi, itatoa ajira 3,000 za moja kwa moja na tayari mafunzo kwa baadhi ya wahudumu 150 wa mahali hapo yameanza.

"Matarajio wakati wowote ndani ya mwezi huu kazi rasmi za uchinjaji wa ng'ombe ndani ya machinjio hii inaweza kuanza, kinachosubiriwa kwa sasa ni kumalizika kwa mafunzo ya wafanyakazi wa machinjio yanayoendelea kutolewa, ila kuhusu ujenzi huo kwa asilimia kubwa kila kitu kimeshakamilika" alisema.

Shauri alisema kwa kuzingatia matakwa ya walaji wa nyama, ng'ombe watachinjwa asubuhi hadi jioni ili kuondoa msongamano unaosababishwa na utamaduni wa kuchinja ngombe usiku pekee.

Alisema wanatarajia kuanzisha kiwanda cha kuchakata nyama katika eneo hilo, kitakachokuwa chini ya kikundi cha akina mama.

Shauri alisema kiwanda hicho kitazalisha nyama za aina mbalimbali zikiwemo za kusaga na zingine kulingana na matakwa ya mlaji kisha kuziingiza sokoni.

"Kiwanda hiki kitakachokuwa kikisimamiwa kwa karibu na uongozi wa jiji, malengo yake ni kuhakikisha kinazalisha nyama aina tofauti tofauti yakiwemo maini, nyama ya nundu na zinginezo kisha kuziweka katika vifungashio maalumu na kumfikia mteja mahali alipo, lakini pia kuzipeleka katika 'Supermarket' kwa ajili ya kuuzwa, huu ni uwekezaji ambao utaongeza ufanisi wa machinjio yetu" alisema.

Shauri alisema pia kutokana na uchunaji wa kisasa jiji hilo na wachinjaji, wanatarajia kuvuna ngozi bora ya ng'ombe, mbuzi , na kondoo hivyo watapata soko zuri tofauti na ilivyokuwa awali.

Aliwataka wafanyabiashara wa nyama wa mkoa wa Dar es Salaam, wajiandae kutumia fursa za machinjio hiyo ya kisasa kwa kuweka mazingira mazuri yatakayowawezesha wananchi kupata nyama kwa ubora ule ule unaozalishwa kutoka machinjioni hapo.

Shauri pia aliwataka wauzaji na wasafirishaji wa ng'ombe, mbuzi, na kondoo kutoka mikoani, wajiandae kuongeza idadi ya mifugo inayoletwa Dar es Salaam, kwa kuwa mazingira ya machinjio hiyo kwa sasa yamekuwa bora kuwezesha zaidi ya mifugo 5,000 kuchinjwa kwa siku.

Scanned with CamScanner